



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA

Unapojuibu tafadhalii taja:

Kumb:HWR/K.2/VOL.IV/12/107

13/03/2023

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P 51,  
Ruangwa

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa anayo furaha ya kutangaza nafasi 01 ya ajira ya kudumu kwa Watanzania wenyе sifa stahiki kwa nafasi ya **Msaidizi wa kumbukumbu Daraja la II**. Nafasi hii ya ajira inatokana na kibali cha ajira mbadala kutoka kwa **Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora** kwa kibali chenye **Kumb. Namba FA.170/372/01"A"/107** cha tarehe **11 Januari, 2023**.

**MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II.**

**A. Sifa za mwombaji:**

- Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne (IV) au Sita (VI) pia awe amehitimu mafunzo ya stashahada "NTA Level 6" katika fani ya Rasimu ramani (cartography) au (geoinformatics), sharia, Afya au Masijala kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

**B. KAZI NA MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II.**

- Kuorodhesha barua zinazoigia Masjala kwenye regista (incoming correspondence register)
- Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi (outcoming correspondence register)
- Kusambaza majalada kwa watendaji(Action Officer)
- Kupokea majalada yanayorudi masjala kutoka kwa watendaji.
- Kutafuta kumbukumbu au nyaraka au majalada yanayoitajika na watendaji

- Kurudisha majalada kwenye shubaka au kabati la majalada(racks/filling cabinet) au mahali pengine yanapoifadhiwa
- Kufuatilia majalada ndani ya Taasisi(file tracking)


### **1. MASHARTI YA JUMLA**

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Mwombaji awe na kitambulisho/namba ya utambulisho wa Uraia kutoka Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA)
- Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa, maelezo binafsi (CV) na nyaraka zote muhimu pamoja na picha mbili (2) (Passport size) zilizopigwa hivi karibuni.
- Testimonials "provisional results" "statement results' hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (**FORM FOUR AND FORM SIX RESULTS SLEEPS) HAVITAKUBALIWA**
- Nafasi ya kazi iliyoombwa iandikwe juu ya bahasha, kutozingatia hii kutasababisha maombi ya kazi kuwa batili
- Kwa wale watakaopita kwenye mchujo wa awali (short listened candidates). Ndio watakaoitwa kwenye usaili (interview) na kufika na vyeti halisi.
- Barua zote za maombi ziandikwe kwa Mkono na kutumwa kwa njia ya posta kwa anwani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA,  
S.L.P 51,  
**RUANGWA**

**NB; Uwasilishaji wa barua za maombi kwa mkono katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya hazitapokelewa.**

**Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ni tarehe 29 Machi,  
2023 saa 9:30 Alasiri.**



Frank F. Chonya  
**Mkurugenzi Mtendaji (W)**

*MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
RUANGWA*

---

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W); Barabara ya Boma; S.L.P 51 RUANGWA, LINDI; Simu: +255 32 933212; Nukush: +255 32 933259; Barua pepe: [info@ruangwadc.go.tz](mailto:info@ruangwadc.go.tz); Tovuti: [www.ruangwadc.go.tz](http://www.ruangwadc.go.tz)